Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.45, - 2025

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# VIJANA WA KITANZANIA VINARA UANDISHI WA INSHA EAC NA SADC

## - KAZI IENDELEE -




**BODI YA UHARIRI**

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Lucas Haule
Fradius Mugoa
Elizabeth Marwa
Dionice Lukweme
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## ELIMU NA MASHINDANO YA INSHA – MBEGU ZA UZALENDO NA UBUNIFU

Mashindano ya uandishi wa insha katika ngazi za kikanda yamekuwa kioo cha kuonyesha namna elimu inavyoweza kuamsha fikra za vijana na kuandaa kizazi kinachoweza kushindana kimataifa kwa hoja na ubunifu. Ushindi wa wanafunzi wetu katika Mashindano ya Uandishi wa Insha za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC, EAC ni ushahidi kuwa Tanzania inazalisha vijana wenye uwezo wa kuchambua masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa upeo mpana.

Ni jambo la kujivunia kuona Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na wadau wa kikanda ikiendelea kusimamia kwa umakini mashindano haya. Hatua hii kielelezo tosha kuwa Serikali imedhamiria kuwekeza katika vipaji vya vijana na kuimarisha ubora wa elimu.

Tunaposhuhudia wanafunzi wakipewa jukwaa la kuandika na kufanya utafiti, tunatambua kuwa Serikali imeweka msingi thabiti wa kujenga kizazi kinachofikiri kwa kina, kinachojenga uzalendo na kinachoweza kuchangia maendeleo ya taifa. Hii ni njia ya kuandaa raia wenye mchango chanya kwa taifa na kwa jumuiya za kikanda.

Tunaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa mashindano haya na kuendelea kutoa tuzo kwa washindi wengi. Hii imeongeza hamasa kubwa kwa wanafunzi kushiriki na imeonyesha kuwa Serikali inathamini kila kipaji.

Ni wajibu wa jamii nzima walimu, wazazi na wadau wa elimu kuunga mkono juhudi hizi ili kuhakikisha kuwa kalama za vijana wetu zinaendelea kuandika historia mpya ya taifa kwa ujasiri, ubunifu na uzalendo.



Mageuzi ya Elimu Nchini >

# SERIKALI YASUKA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MAGEUZI YA ELIMU NCHINI

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa elimu inaendelea kutekeleza mikakati kabambe ili kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 kwa mafanikio.

Akifunga Mkutano wa Mwaka wa Tathmini ya Pamoja ya Sekta ya Elimu 2024/25 jijini Dodoma Oktoba 24, 2025, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amesema Serikali inajivunia mafanikio mengi katika sekta ya elimu na imejipanga kuongeza fursa za kuboresha elimu, ikiwemo kuongeza idadi ya walimu wa sayansi, biashara na masomo ya ufundi.

**"Tutaimarisha na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya elimu"** amesema Katibu Mkuu.

Amewashukuru wadau wote kwa ushirikiano mzuri na amewapongeza walimu wote wa ngazi mbalimbali kwa kazi nzuri wanayofanya.

"Hakuna elimu bila mwalimu, kwani ndio msingi wa kujenga nguvu kazi ya Tanzania yenye maarifa na ujuzi na kuwa tayari kushinda katika soko la ajira kitaifa na Kimataifa" Ameeleza Prof. Nombo.



**Prof. Carolyne Nombo**
Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Elimu) Ndg. Atupele Mwambene amesema Mkutano huo umekuwa nyenzo kubwa ya wadau mbalimbali kuchangia maoni yao ya kitaalam ambayo yatawezesha kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Sera ya Elimu.



**Ndg. Atupele Mwambene**
Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI

**"Sisi kama sekta ya elimu bado tuna fursa za kufanya vizuri zaidi, kwa kuboresha na kuimarisha utendaji katika upande wa elimu ya awali, Msingi na Sekondari ili tuongeze fursa za upatikanaji wa elimu kwa vitendo"** amesema Mwambene.

> **"**
> ***Hakuna elimu bila mwalimu, kwani ndio msingi wa kujenga nguvu kazi ya Tanzania yenye maarifa na ujuzi***



Uandishi wa Insha >

# VIJANA WA KITANZANIA VINARA UANDISHI WA INSHA EAC NA SADC



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Omari, amesema Serikali itaendelea kuwekeza katika kukuza vipaji vya vijana kupitia elimu, akisema juhudi hizo zinawajenga kuwa kizazi kinachofikiri kwa kina na chenye mchango kwa taifa.

Dkt. Omari ameyasema hayo Oktoba 26, 2025 jijini Dodoma, wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa washindi wa mashindano ya uandishi wa insha za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC, ambapo wanafunzi kutoka shule mbalimbali walipewa zawadi kwa ubunifu na uwezo wao wa kuandika.

Amesema mashindano hayo yanasaidia kujenga uzalendo miongoni mwa vijana na kuwahamasisha kutumia teknolojia kwa njia chanya inayokuza fikra tunduizi. Amewapongeza walimu na wazazi kwa kuwaandaa vizuri wanafunzi na amewahimiza wanafunzi nchini kote kuendelea kushiriki mashindano kama haya ili kukuza vipaji vyao zaidi.

**"Tunawafundisha vijana kufikiri zaidi, jambo ambalo litakuwa tunda jema kwa kizazi kijacho. Hii ni njia mojawapo ya kukuza uzalendo na kuwaandaa kuwa raia wenye mchango chanya kwa taifa,"** amesema Dkt. Omari.

Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa,amesema mashindano hayo yamechochea na kukuza umahiri wa wanafunzi katika uandishi, utafiti, na ufahamu mpana wa masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika jumuiya hizo mbili za kikanda.

Pia amewapongeza washindi wote wa kitaifa na kikanda, akiwemo Hollo Alice Kadala kutoka Shule ya Sekondari Msalato, aliyeshika nafasi ya tatu kitaifa na ya tatu kikanda katika mashindano ya SADC mwaka 2023, pamoja na Blandina Kabalemesa wa Shule ya Sekondari Anwarite, aliyeshika nafasi ya kwanza kitaifa na ya nne kikanda katika mashindano ya EAC mwaka 2024.

Naye, Mratibu wa Insha kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Bi. Matuha Masati ameipongeza Sekretarieti ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za SADC Kwa kuendesha Mashindano ya Uandishi wa Insha kwani yamekuwa chachu Kwa vijana kufanya utafiti,kujifunza na kufahamu vizuri mchakato na hatua mbalimbali za uimarishaji Kwa nchi wanachama.

Mashindano hayo husimamiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) kwa insha za nchi za Afrika Mashariki (EAC) na za SADC husimamiwa na Wizara ya Elimu kwa upande wa Tanzania bara na Zanzibar.

Jumla ya wanafunzi 1,096 walishiriki katika mashindano ya uandishi wa insha za EAC na SADC mwaka 2023, wakiwemo wanafunzi 557 wa EAC na 539 wa SADC, huku mwaka 2024 ukishirikisha wanafunzi 892, kati yao 243 wa SADC na 649 wa EAC.



Lishe Shuleni >

# MPANGO WA LISHE SHULENI WAIMARIKA - DKT. MTAHABWA



**Dkt. Lyabwene Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

> ***Ajenda ya chakula shuleni ni muhimu na ina mchango mkubwa katika kuinua kiwago cha elimu na kuboresha ustawi wa wanafunzi.***

Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa amesema kuwa Serikali ya Tanzania inatambua kuwa ajenda ya chakula shuleni ni muhimu na ina mchango mkubwa katika kuinua kiwango cha elimu na kuboresha ustawi wa wanafunzi.

Dkt. Mtahabwa amesema hayo Oktoba 22, 2025 jijini Dodoma akijibu maswali ya washiriki mbalimbali katika Mkutano wa Mwaka wa Tathmini ya Sekta ya Elimu, ikiwemo Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Viziwi Dodoma Mary Mussa na John Ndonde ambao pamoja na kupongeza juhudi mbalimbali katika uboreshaji wa miundombinu pia walitaka kujua mikakati inayotekelezwa kuimarisha huduma ya chakula shuleni.

Kamishna huyo ameongeza kuwa kutambua umuhimu huo, Serikali inatekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe Shuleni, na sasa kiwango cha shule kupata chakula kimeongezeka kufikia asilimia 61.

Aidha, amebainisha kuwa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mwongozo wa Elimu ya Kujitegemea, unaolenga kuwashirikisha wanafunzi moja kwa moja katika shughuli za upatikanaji wa chakula na lishe bora. Mwongozo huo pia unalenga kuimarisha ujuzi wa kazi za mikono kama vile kulima bustani na shughuli za ufugaji.

**"Watoto wanapaswa kupewa nafasi ya kujifunza kwa vitendo kupitia shughuli kama kilimo cha mbogamboga shuleni, ili kuwajengea ujuzi wa kujitegemea na kuchangia katika upatikanaji wa chakula hicho"** amesema Dkt. Mtahabwa.



Tathmini ya Sekta ya Elimu >

# WANAFUNZI WASHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA TATHMINI YA SEKTA YA ELIMU YA MWAKA 2025



Wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari wameshiriki kikamilifu katika Mkutano Mkuu wa Tathmini ya Pamoja ya Sekta ya Elimu, ambapo wameipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, wakisema hatua hiyo imeimarisha mazingira ya kujifunza na kufundisha.

Akizungumza katika Mkutano huo Oktoba 24, 2025 jijini Dodoma, Mohammed Saidi kutoka Shule ya Msingi Dodoma, ambaye ni mwanafunzi mwenye mahitaji maalum, amesisitiza umuhimu wa kuwajali wanafunzi kama yeye kwa kuwapatia vitabu, viti mwendo, walimu mahiri na kutambua vipaji vyao.

Nenelo Mdachi wa Shule ya Sekondari Viwandani na Zaituni Halfan wa Sekondari Nzuguni walihimiza kushughulikia changamoto za kimaadili miongoni mwa walimu. Wamesisitiza utekelezaji wa Mwongozo wa adhabu ili kuimarisha nidhamu, maadili na taaluma shuleni.

Mohamod Idi kutoka Sekondari Umonga ametoa wito wa kuongezwa kwa walimu wa Sayansi na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mkondo wa Amali. Amesema mkondo huo unasaidia kukuza maarifa ya vitendo na kuandaa wataalamu wa baadaye.



Fursa za Elimu >

# SERIKALI YAONGEZA FURSA ZA ELIMU KWA WENYE MAHITAJI MAALUMU

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Maalum, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Magreth Matonya amesema Serikali inaendesha programu mbalimbali za elimu, ikiwemo ya kubaini wanafunzi wenye mahitaji maalum kuanzia ngazi ya kijiji kwa ajili ya maandalizi ya kujiunga na shule.

Akizungumza Oktoba 22, 2025 jijini Dodoma katika Mkutano wa Mwaka wa Tathmini ya Pamoja ya Sekta ya Elimu 2024/25, Dkt. Matonya amesema zoezi hilo linasimamiwa na Maafisa Elimu Maalum wa mikoa kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi mbalimbali. Ameeleza kuwa Serikali pia inatekeleza Mwongozo wa Shule ya Nyumbani, ambapo walimu huwafikia wanafunzi nyumbani kila Ijumaa kwa ajili ya kujifunza, kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya mazoezi ya kielimu.

Aidha, amesema kuna ongezeko kubwa la mwamko wa wazazi kuhusu elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum, ambapo tangu mwaka 2020 idadi ya wanafunzi hao imeongezeka kwa zaidi ya mara tatu, ikionyesha mabadiliko chanya katika mtazamo wa jamii kuhusu elimu jumuishi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, katika Wizara hiyo, Dkt. Fredrick Salukele, amesema kuwa Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia katika shule za amali na vyuo vya ufundi nchini. Ameeleza kuwa kuna mipango miwili mikuu inayotekelezwa kwa lengo hilo.

Mpango wa kwanza unahusisha Mradi wa Education Skills for Productive Jobs - Awamu ya Pili, ambapo Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia kwa shule za amali 103 zinazijengwa, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) 54, pamoja na Vyuo vya VETA 65 vinavyojengwa na vyuo 25 vya vilivyokamilika.

Mpango wa pili unatekelezwa kupitia bajeti ya Wizara, ambapo fedha zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia katika shule za sekondari pamoja na shule 29 za ufundi. Kwa ujumla, takriban Shilingi bilioni 39 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.



**Dkt. Magreth Matonya**
Mkurugenzi wa Elimu Maalumu



**Dkt. Fredrick Salukele**
Mkurugenzi wa Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi

Dkt. Salukele amesema hatua hizi ni sehemu ya jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, ili kuongeza ujuzi na maarifa kwa wanafunzi wanaosomea fani mbalimbali za ufundi stadi.



Utekelezaji Mageuzi ya Elimu >

# SERIKALI KUSHIRIKIANA NA WADAU KUTEKELEZA MAGEUZI YA ELIMU




**Prof. Daniel Mushi**
Naibu KAtibu Mkuu Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu

> **"*Serikali inaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023*"**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, amesema kuwa Serikali inaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi mahitaji ya sasa na baadae ya kijamii na kiuchumi.



Prof. Mushi ameeleza hayo Oktoba 22, 2025 jijini Dodoma akizungumza na Waandishi wa Habari baada ya kufungua Mkutano wa Mwaka wa Tathmini ya pamoja ya Sekta ya Elimu, 2024/25 unaolenga kutathmini mafanikio yaliyopatikana, kubaini changamoto na kupanga mikakati kabambe ya utekelezaji wa mageuzi ya elimu.

Ameongeza kuwa, katika kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia, Serikali kupitia Wizara imejielekeza katika kukuza elimu inayolenga kutoa maarifa na ujuzi unaohitajika katika karne ya 21, ili kuliwezesha taifa kupata wahitimu mahiri wanaoweza kushindana kikamilifu katika soko la ajira la ndani na kimataifa.

"Kuna ongezeko la rasilimali, ongezeko la miundombinu, Serikali haiwezi peke yake kuwezesha mahitaji haya yote, ndiyo maana inakutana na wadau mbalimbali kujadili na kupanga juu ya maeneo na namna nzuri ya kuwekeza katika elimu ili kufikia lengo la kuandaa rasimali watu mahiri ambao ni mtaji mkubwa katika kufikia Dira 2050," amesema Prof. Mushi.

Pongezi kwa Mageuzi ya Elimu >


# WADAU WA ELIMU WAIPONGEZA SERIKALI KWA KUTEKELEZA MAGEUZI YA ELIMU

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uingereza, Godfrida Magubo, ameipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu katika ngazi zote za elimu ambayo imechochea ufundishaji na ujifunzaji.

Magubo amesema hayo Oktoba 22, 2025 jijini Dodoma katika Mkutano wa Mwaka wa Tathimini ya Sekta ya Elimu, ambapo amesisitiza matumizi ya teknolojia na takwimu sahihi ili kuwezesha kufuatilia maendeleo ya elimu. Ameahidi kuwa Serikali ya Uingereza itaendelea kushirikiana na Serikali katika kukuza elimu jumuishi na endelevu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Simon Nanyaro, amesema Mkutano huo ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha uwazi, uwajibikajina ufanisi katika utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya elimu.

> ***"Serikaliya Uingereza itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kukuza elimu jumuishi na endelevu.***




**Mhe. Godfrida Magubo**
Mwakilishi wa Ubalozi wa Uingereza

Mwakilishi wa Jumuiya za Kidini kutoka Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Dkt. Joyce Mboya, amesema kama wadau muhimu wapo tayari kushirikiana na Serikali kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu bora itakayomwandaa kwa maisha na kazi.



Elimu na Uchumi >

# KAMPASI YA NJOMBE KUCHOCHEA MAENDELEO YA ELIMU NA UCHUMI NYANDA ZA JUU KUSINI

Kuanzishwa kwa Kampasi ya Njombe ya Chuo Kikuu cha Dodoma kupitia Mradi wa HEET kumeanza kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu, ajira na uchumi wa mkoa wa Njombe. Mradi huu unalenga kuongeza fursa za elimu ya juu kwa vijana wa Kusini na kuchochea maendeleo ya miundombinu ya kisasa.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, akizungumza na na viongozi wa Mkoa wa Njombe akiwemo Mkuu wa Mkoa Mhe. Anthony Mtaka, Katibu Tawala na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Amesema Njombe imepata fursa ya kipekee kwa kuwa na matawi ya vyuo vikuu zaidi ya kimoja.

Prof. Nombo ameeleza kuwa uwepo wa kampasi hiyo utachochea shughuli za kiuchumi katika maeneo jirani. Amesisitiza umuhimu wa kujenga nyumba za makazi, hosteli za wanafunzi, na vituo vya huduma kama maduka na migahawa ili kuandaa mazingira rafiki kwa wanafunzi na watumishi wa kampasi hiyo.



**Prof. Carolyne Nombo**
Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Ameongeza kuwa ongezeko la wanafunzi litahitaji huduma bora za afya, usafi wa mazingira, Miundombinu ya TEHAMA. Alitoa wito kwa taasisi husika kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa wakati katika eneo la Mradi kabla ya kuanza Kwa udahili wa Wanafunzi hasa kwa kuzingatia mfumo wa "blended learning" unaotegemea miundombinu ya intaneti ya uhakika.

Prof. Nombo ameupongeza Mkoa huo kwa ushirikiano wake katika utekelezaji wa miradi ya elimu. Aliahidi kuwa Wizara itaendelea kushirikiana na mkoa huo kuhakikisha mradi wa Kampasi ya Njombe unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.



Mafunzo ya Ulinganifu >

# ESWATINI WAJA TANZANIA ZIARA YA MAFUNZO YA ULINGANIFU KATIKA SEKTA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



**Prof. Daniel Mushi**
Naibu KAtibu Mkuu Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepokea ujumbe wa wataalamu kutoka Falme ya Eswatini ambao wapo katika ziara ya mafunzo ya ulinganifu, inayoratibiwa na taasisi ya Economic Policy and Analysis Research Centre (ESEPARC) kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Hifadhi ya Jamii (MoLSS) ya Falme ya Eswatini.

Ziara hiyo imefanyika kuanzia tarehe 13 Oktoba 2025, ikiwa na lengo la wataalamu wa nchi hiyo, kupata uzoefu kutoka Tanzania wa utekelezaji wa programu za maendeleo ya ujuzi, ikiwa ni sehemu maandalizi ya mpango kabambe wa kukuza ujuzi katika Nchi hiyo.

Akizungumza na ujumbe huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, amesema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kusimamia na kuratibu utoajiwa elimu nchini, kuandaa Sera, Sheria na miongozo mbalimbali kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi elimu ya juu. Lengo kuu likiwa kuandaa wahitimu wenye maarifa, stadi na ujuzi.

Aidha, Prof. Mushi amebainisha kuwa Wizara pia inasimamia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na kuimarisha matumizi yake katika sekta mbalimbali zikiwemo biashara, viwanda, kilimo na afya.

Ili kufikia malengo mkazo umewekwa katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata mafunzo ya kumjengea ujuzi utakaomwezesha kujiajiri au kuajiriwa, jambo linalochochea ukuaji wa uchumi na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.

Kwa upande wake, Bi. Gcebile Dlamini, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mipango na Maendeleo ya Rasilimali Watu kutoka Eswatini ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwapa fursa ya kujifunza njia bora za uendeshaji wa elimu na maendeleo ya ujuzi, kwani Tanzania imepiga hatua kubwa katika maeneo hayo.

> “ ***Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu nchini, kuandaa Sera, Sheria na miongozo mbalimbali kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi elimu ya juu.***



Usimamizi Miradi ya Elimu >

# SERIKALI YASISITIZA USIMAMIZI MAKINI WA MIRADI YA ELIMU ILI KULINDA RASILIMALI ZA UMMA



**Mhe. Abdul Maulid**
Mkurugenzi wa Elimu Msingi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolokia

Serikali imewataka viongozi wa usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi hiyo ili kulinda rasilimali za umma na kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana.

Akifungua mafunzo ya usimamizi wa ujenzi kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST), kwa niaba ya Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Elimu Msingi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolokia Abdul Maulid amesema ripoti za Mdhibiti na baadhi ya miradi, hivyo kila Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zimebainisha mapungufu katika hatua ya ujenzi lazima ikaguliwe na wataalamu wa halmashauri.

Maulid amesisitiza hayo Oktoba 11, 2025 Mkoani Morogoro, amesema kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila mtoto anajifunza katika miundombinu bora, hivyo miradi ya ujenzi lazima ifuate viwango vilivyowekwa.

Pia amewataka viongozi, shule na jamii kuanzisha utaratibu wa ukarabati mdogo kupitia ruzuku za uendeshaji ili kuzuia uchakavu wa mapema na kudumisha miundombinu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI ameeleza kuwa mafunzo hayo yanawahusisha washiriki 3,202 kutoka mikoa ya Morogoro, Iringa, Arusha na Mwanza, yakilenga kuboresha usimamizi wa miradi na kuhakikisha thamani ya fedha.

Amesema kuwa Serikali imetumia Sh. bilioni 311.3 katika miaka ya fedha 2022/23 na 2023/24 kwa ujenzi na ukarabati wa shule, ikijumuisha madarasa, vyoo, mabweni, nyumba za walimu, majengo ya utawala na shule mpya 46.



> ***"Serikali imetumia Sh. bilioni 311.3 katika miaka ya fedha 2022/23 na 2023/24 kwa ujenzi na ukarabati wa shule***

Vifaa vya Mafunzo VETA >

# SERIKALI YAKABIDHI VETA VIFAA VYA MAFUNZO VYENYE THAMANI YA SHILINGI BILIONI 8.4, VYUO 63 KUNUFAIKA




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amekabidhi rasmi vifaa vya mafunzo vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.4 kwa vyuo 63 vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika Oktoba 17, 2025 jijini Dar es Salaam, wakati wa Mkutano wa VETA na Wamiliki wa Viwanda, Waajiri pamoja na Wadau wa Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Prof. Nombo amesema kuwa vifaa **hivyo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa vitendo.**

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera, amesema Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea ujuzi wa ndani kupitia ushirikiano wa kimkakati kati ya Wizara husika.

Ameeleza kuwa VETA imekuwa nguzo muhimu ya mabadiliko ya kiufundi katika sekta mbalimbali. Sekta hizo ni pamoja na uzalishaji, kilimo, nishati na madini. Aidha, VETA pia inachangia katika maendeleo ya teknolojia na ujenzi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), CPA Antony Kasore, amesema kuwa VETA itaendelea kuimarisha ushirikiano kati yake na wamiliki wa viwanda na wadau wa sekta ya ufundi stadi ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi mahitaji ya soko la ajira.

CPA Kasore ameishukuru Serikali kwa kuimarisha miundombinu ya VETA na **kuongeza vyuo vya VETA kutoka 37 hadi 80 vinavyofanya kazi, huku vyuo vingine 65 vikiwa katika hatua za kukabidhiwa.**



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

-----------------------------------------

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

-----------------------------------------

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

-----------------------------------------

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

-----------------------------------------

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi,
Muhimbili (MUHAS),
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

-----------------------------------------

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

-----------------------------------------

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

-----------------------------------------

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

-----------------------------------------

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
**27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,**
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

-----------------------------------------

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

-----------------------------------------

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

-----------------------------------------

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

-----------------------------------------

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz

**- KAZI IENDELEE -**